Kuabudu Katika Siku Ya Bwana

na

Ellis P. Forsman

Kuabudu Katika Siku Ya Bwana

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 8, 2011

Kuabudu katika Siku ya Bwana

Matendo 20: 1-16

Kanisa la Bwana Yesu linakutana siku ya kwanza ya juma kwa ajili ya ibada. Wakati huo tunakula meza ya Bwana kwa kukumbuka kifo na kufufuka kwa Yesu. Pia ni wakati wa kuimizana na kufundishana neno la Mungu, kuimba na kuomba kwa Mungu, na kutoa kile tulichokipata ili kuendeleza kazi ya Bwana.

Kanisa la Bwana lina kutana siku za juma pili kwa ajili ya sababu muhimu.

Kwa Nini Kuabudu Siku ya Juma Pili?

Kwanza, kanisa lina abudu siku za Jumapili kwa sababu vitu muhimu vilitendeka siku iyo.

Yesu alifufuka siku ya kwanza ya juma.

Marko 16:9, "*Naye alipofufuka alfajiri siku ya kwanza ya juma, alimtokea kwanza Mariamu Magdalene, ambaye kwanza alimtoa pepo saba."*

Roho Mtakatifu akawashukia mitume siku hiyo.

Matendo 2:1-4, *"Hata ilipotimia siku ya Pentekoste walikuwako wote mahali pamoja. Kukaja ghafla toka mbinguni uvumi kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi. Kukawatokea ndimi zilizo gawanyikana, kama ndimi za moto ulitowakalia kila mmoja wao. Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyo wajalia kutamka."*

Siku hii ya "Pentekoste" kimsingi inamaanisha "siku hamsini." Ilikuwa ni sikukuu kuu ya sheria ya Wayahudi ambayo ingesheherekewa siku hamsini baada ya sikukuu ya Pasaka.

Walawi. 23:11, 15, "*Naye atautikisa mganda mbele za BWANA ili kwamba ukubaliwe kwa ajili yenu; siku ya pili baada ya sabato kuhani atautikisa."*

Inatakiwa "*iwe kesho, baada ya sabato."*

Sasa, siku ambayo mitume walipokea Roho Mtakatifu ilikuwa ni siku ya juma pili.

Kanisa la Bwana wetu Yesu Kristo lilianzishwa Sikuhiyo.

Matendo. "*Walipoyasikia haya wakachomwa mioyo yao, wakamwambia Petro na mitume wengine; tutendeje ndugu zetu? Petro akawaambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie. Akawashuhudia kwa maneno mengine mengi sana, na kuwaonya akisema, jiokoeni na kizazi hiki chenye ukaidi. Nao waliolipokea neno lake wakabatizwa; na siku ile wakaongezeka wapata watu elfu tatu. Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali.*"

Walizidishwa pamoja katika ushirika na wakaanza kufanya uinjilisti ulimwenguni kote. Katika wakati huu kuendelea katika Agano Jipya, mtu anaweza kuona mabadiliko, kwa sababu kanisa la Bwana lilikuwepo.

Kanisa lili kutana siku ya juma pili kukumbuka, katika chakula maalum, kifo na kufufuka kwa Yesu Kristo.

Matendo. 20: 7, "*Hata siku ya kwanza ya juma tulipokuwa tumekutanika ili kuumega mkate, Paulo akawahutubu, akiazimu kusafiri siku ya pili yake naye akafuliza maneno yake hata usikua wa manane.*"

Makanisa ya Kristo yaliendelea kukutana miaka yote siku za juma pili, na walipewa maagizo kuhusu mambo mengine.

Waliambiwa ku "weka pembeni" katika siku hii ya kwanza.

1 Wakor. 16:1-2, *"Kwa habari ya ile changizo kwa ajili ya watakatifu, kama vile nilivyoamuru makanisa ya Galatia, nanyi fanyeni hivyo. Siku ya kwanza ya juma kila mtu kwenu na aweke akiba kwake kwa kadiri ya kufanikiwa kwake, ili kwamba michango isifanyike hapo nitakapokuja."*

Walipaswa kutumia muda huu "kuimiza moja baada ya mwingine."

Waeb. 10:25-26, *"Wala tusiache kukusanyika pamoja kama ilivyo desturi yaw engine; bali tuonyane na kuzidi kufanya hivyo, kwa kadiri mwonavyo siku ile kuwa inakaribia. Maana kama tukifanya dhambi*

kusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile kweli; haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi."

Wanafunzi wa Biblia wametafsiri maana ya neno kukutana siku ya kwanza ya juma katika kiyunani kiukweli ni kukutana siku ya kwanza ya wiki ya kila wiki.

Wakristo wa kwanza hawakushiriki meza ya Bwana siku nyingine yo yote isipokuwa siku ya kwanza ya juma.

Inachozungumzia kuvunja mkate kila siku, lakini kwamba Wakristo wa kwanza walikutana mara nyingi na kushiriki chakula cha Bwana pamoja. "*kumega mkate*" ilikuwa ni neno lililo tumika katika kula chakula. Agizo la kushiriki meza ya Bwana ilikuwa ni siku ya kwanza ya juma.

Paulo alikuwa katika haraka ya kurudi Yerusalem kwa muda muafaka siku ya Pentekoste. Alifika Troa siku ya juma nne, lakini hakuendelea na safari hadi juma tatu iliyo fuata kwa sababu alitaka kukutana na ndugu pale katika siku ya kwanza ya juma walipokutana ili kumega mkate. Alikuwa na mengi ya kusema kwa kusanyiko lote kwa hiyo aliongea hadi usiku wa manane wakashiriki mkate; alafu akaendeleza maneno yake mpaka jioni siku ya juma tatu kabla hajaendelea na safari yake kwenda Yerusalem.

Paulo hakuwaambia ili wawe na mkutano huu wa kipekee katikati ya wiki. Kwa kufanya hivyo ingekuwa ni nyongeza katika agizo la Bwana kukutana siku ya kwanza ya juma ili kumega mkate.

- Matendo. 20:6-7, *"Sisi tukatweka baada ya siku za mikate isiyotiwa chachu, tukatoka Filipi, tukawafikia Troa, safari ya siku tano, tukakaa huko siku saba. Hata siku ya kwanza ya juma tulipokuwa tumekutana ili kuumega mkate, Paulo akawahutubu akiazimu kusafiri siku ya pili yake, naye akafuliza maneno yake hata usiku wa manane."*

- Matendo. 20: 16, *"Kwa sababu Paulo amekusudia kupita Efeso merikebuni, asije akakawia katika Asia; kwa maana alikuwa na haraka, akitaka kuwahi Yerusalemu siku ya Pentekoste, kama ikiwezekana."*

Wakristo wa kwanza walikutana kila siku, lakini hiyo ilikuwa makundi madogo walipokwenda nje wawili kwa watatu kuhubiri injili katika nyumba za watu hao. Walipofanya hivi walikuwa pia na vyakula katika nyumba hizi, lakini hakuwa chakula cha Bwana.

Kulikuwa na mkutano wa kila siku katika hekalu la Wayahudi ili kujifunza sheria ya Kiyahudi, lakini maagizo kuhusu sabato haikutumiwa katika mikutano hii.

Siku hizi tunaweza tukawa na mikutano ya kila siku, lakini haikuwa kwa kusudi la kushiriki meza ya Bwana.

Pili, makanisa ya Kristo yanaabudu siku ya Juma Pili kwa sababu ya mipangilio muhimu.

Yesu alisema wakati wanafunzi wake walipo kwenda ulimwenguni mwote, walitakiwa kuwafundisha wanafunzi *".....kuyashika yote niliyowaamuru ninyi na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari."* (Math. 28:20).

Kwa hiyo mtu anapoona makanisa ya kwanza yana shiriki meza ya Bwana siku ya kwanza ya juma, ilifuatia kwamba mitume waliwafundisha kufanya hivyo. Kama mitume waliwafundisha kumega mkate siku ya kwanza ya juma, ilifanyika ili kufuata agizo la Yesu. Sasa, mifano ya makanisa katika Agano Jipya ni muhimu, walipokuwa wakifundishwa binafsi na mitume.

Tatu, uthibitisho wa wanahistoria umetanda kwamba makanisa yalikutana siku za juma pili kwa ajili ya ibada kwa heshima ya Kristo.

Ignatius wa Antiokia, mwana historia aliyejirudia, aliishi kati ya miaka 37 A.D na 108 A.D. aliandika kitabu kiitwacho, "Kila rafiki wa Kristo atunze siku ya Bwana kama Sikukuu, siku ya ufufuo, malkia na kuhani wa siku zote (za juma).

Justin Martyr aliyeishi kati ya miaka 100 na 165 A.D. aliandika, "Na katika siku iliyoitwa Juma Pili, wote wanaoishi katika miji na nchi wakatane pamoja...mkate na (uzao wa mzabibu) zinaletwa...kuna mchango kwa kila mmoja, na ushirika wa huo ambao shukurani imeshatolewa...Pili ni siku ambayo wote tunkuwa katika mkutano wa siku zote, kwa sababu ni siku ambayo Bwana wetu Yes Kristo alifufuka katika wafu." Justine anaonyesha matendo ya kanisa la kwanza inavyo endelea katika karne ya pili.

Sabato ya Agano La Kale

Kuto. 20:8, “uikumbuke sabato, uiweke takatifu.”

Hili agano walipewa Waisraeli peke yao.

Iilikuwa ni kumbukumbu kati ya Mungu na Israeli.

Kuto. 31:17, *“Ni ishara kati ya mimi na wana wa Israeli milele; kwani kwa siku sita BWANA alifanya mbingu na nchi, akastarehe kwa siku ya saba na kupumzika.”*

Ilikuwa ni siku ya saba, siku ambayo Wayahudi walipaswa kupumzika.

Kutoka. 20: 9-10, *“Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; lakini siku ya saba ni sabato ya BWANA, Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yoyote, wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya malango yako.”*

Wakristo wanapaswa kutunza siku ya kwanza ya juma takatifu.

- Waeb. 10:25-26, *“Wala tusiache kukusanyika pamoja kama ilivyo desturi yaw engine; bali tuonyane na kuzidi kufanya hivyo, kwa kadiri mwonavyo kuwa siku ile kuwa inakaribia. Maana kama tukifanya dhambi kusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi.”*
- Waeb. 10: 27-29, *“Bali kuna kuitazamia hukumu yenye kutisha, na ukali wa moto ulio tayari kuwala wao wapingao. Mtu aliyeidharau sheria ya Musa, hufa pasipo huruma kwa neno la mashahidi wawili au watatu. Mwaonaje? Haikumpasa adhabu iliyo kubwa zaidi mtu Yule aliyemkanyaga mwana wa Mungu na kuihesabu damu ya agano iliyotakaswa kwayo kuwa ni kitu ovyo, na kumfanyia jeuri Roho wa neema?”*

Adhabu kwa Myahudi ye yote aliyekuwa hatunzi Sabato alipigwa mawe.

Onyo kwa Wakristo katika barua ya Waebrania walio chukuwa mkutano wa siku ya kwanza ya juma kimzaha anajiweka mwenyewe katika adhabu ya hatari. Paulo anaonyesha katika barua yake kwamba hili ni jambo la msingi.

Wakristo wanatakiwa kuchunguza kwa makini mambo haya wakati siku ya kwanza ya juma inapofika.